# IMANI GANI?

***"…Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana" Waebrania 11:1.*** Kwa maneno mengine ni kusema; Imani ni kukubali mambo yaliyoahidiwa kuja ambayo bado hayajatimia kwa sasa; ila bila shaka yanakuja kuwa. Kwa sababu hii; wafuasi wa imani ile waliyonayo wanaishi katika uhakika wa matarajio ya yale waliyoyakubali. Kristo kupitia kwa Paulo anayathibitisha haya akisema; ***"…kitu kilichotarajiwa kikionekana, hakuna taraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho? Bali tikikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi" Warumi 8:24-25.***

Kwa maneno hayo basi; sasa tunakuja katika swali la mada yetu. Wote wamwabuduo Mungu wanadai kuwa na imani kwake. Na hili ni matokeo ya agizo la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba watu wanapaswa ***"kumwamini Mungu" {soma Marko11:22}.*** Basi kwa vile imani ni kukubali na kuamini katika yale yaliyoahidiwa; ambako huku kukubali na kuamini kunathibitishwa kwa kufanya yale ambayo mtoa ahadi ameelekeza; twauliza sasa; ni jambo gani hilo aliloelekeza Mungu, ambalo hatujaliona bado, lakini twalikubali na kuliamini? Kivyovyote vile; linapaswa kuhusu kusudi la Mungu kutuumba. Ni lazima pia kuwe na jambo linaloharibu ukubali wa kile Mungu anachoelekeza. Kwa hivyo; ikiwa tutakuwa na imani halisi kweli kwa Mungu; ni sharti tuwe katika nafasi ya kutofautisha kati ya kusudi la Mungu kwetu na taratibu zake; na huu mwingine mbadala wa uharibifu.

## KWANINI MWANADAMU?

Sote tunafahamu kuwa tupo hapa kwa kusudi pekee la kuumbwa zaidi ili tufanywe kuwa viumbe wa roho na kuja kupewa utawala wa hii dunia *{kwa maelezo ya kina kuhusu hili; agiza ujumbe wetu usemao,* ***"KUSUDI LA MWILI";*** *tutakutumia bure}.* Mara uumbwaji wetu utakapokamilika, tutakuwa kama Mungu alivyo hasa; kama alivyokusudia *"kumuumba mtu kwa mfano na sura yake ili mtu huyo akatawale juu ya nchi"* ***{soma Mwanzo 1:26}.*** Jambo hili linatufanya kuhitaji ufahamu kuhusu kitu gani tupaswacho kufanya hivi sasa, ambacho kitatupeleekea kuwa kama Mungu, na ambacho ndicho tunapaswa kuwa na imani nacho.

Katika huu mwili wa damu na nyama, Mungu ametufanya tusio na silika *{yaani, ufahamu wa kuzaliwa nao kama wa wanyama},* wala tusioweza kutengeneza ufahamu wetu wenyewe. Kwa hivyo; ili tuwe na ufahamu wa nini afanyacho Mungu katika maisha yetu ili kutufanya kama yeye; ni lazima tuupate katika chanzo fulani. Mungu alimuumba mtu mwenye akili yenye roho ndani yake *{ila si roho takatifu, wala mtu wa roho ndani ya mwili wa damu na nyama; soma Ayubu 32:8}.* Bwana wetu Yesu Kristo analiweka wazi zaidi jambo hili kuwa hiyo roho inahitaji kuunganishwa na roho nyingine *{iliyo takatifu, ama ya uovu}* ili kuipa ufahamu. Anatuambia akisema; ***"Roho*** *{takatifu}* ***mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu*** *{ama*

*kutia ufahamu ndani ya roho zetu [Ayubu 32:8] na kutufanya kufahamu}* ***ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" Warumi 8:16.*** Hili ni jambo lile lile alilolizungumzia Mungu kupitia kwa Ayubu akisema; ***"…imo roho ndani ya mwanadamu, Na pumzi za Mwenyezi huwapa akili" Ayubu 32:8.***

Sasa basi; yeye Muumbaji, ambaye pekee ndiye ajuaye kile afanyacho katika kumfanya mtu kuwa kama yeye; ni sharti roho yake *{takatifu}* iungane na roho zetu kutupa ufahamu kuhusu mchakato huo. Kwa vile Mungu yuko hivyo alivyo kwa hiari yake mwenyewe *{yuko alivyo bila shuruti yo yote}*; ametuumba sisi pia wenye uhuru wa kuchagua. Baada ya kutuumba katika mwili huu wa damu na nyama, pale Adamu alipokuwa si mtakatifu wala si mwovu; bali awe kile atakachochagua *{mtakatifu, au mwovu}*; Mungu alimruhusu *{na anaturuhusu sisi sasa}* kuchagua *{soma Mwanzo 2:15-17; na kwa maelezo zaidi agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MCHAKATO WA UUMBWAJI WA MTU",*** *tutakutumia bure}.*

## UCHAGUZI WA ADAMU

Tafadhali kumbuka kwamba Mungu ananena na wewe, si na Adamu. Kumbuka kila mmoja wetu anapaswa kujipima mwenyewe kupitia ujumbe huu, ili kujihakikisha kwamba yuko katika imani halisi ama katika imani ya bure na kujidanganya.

Basi kumbukeni kwamba; ***"Imani chanzo chake ni*** *{ama huja kwa}* ***kusikia*** *{yaani kupata ufahamu}****; na kusikia huja kwa neno la Kristo*** *{yaani kupata maelekezo}****" Warumi 10:17.*** Basi ni maelekezo hayo ayapatayo mtu kwamba mtu huyo anajenga imani juu yake inayothibitishwa kwa kufanya sawasawa na hilo aliaminilo *{yaani, kwa mwenendo mzima wa mtu}*; maana, imani pasipo matendo imekufa ***{soma Yakobo 2:26}.***

Sasa basi; je! Adamu alichagua nini na kutoka kwa nani? *{kwa maelezo ya kina zaidi; agiza ujumbe wetu usemao,* ***"MITI MIWILI",*** *utatumiwa bure}.* ***"Basi nyoka*** *{yaani, Shetani; soma Ufunuo 12:9}* ***alikuwa mwerevu…akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa" {soma Mwanzo 3:1-5}.*** Mungu alimwambia Adamu kwamba atakufa endapo atakula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Hayo ni maelekezo ya Mungu. Shetani akaja kinyume cha hayo akimwambia Adamu; ***"Hakika hamtakufa".*** Ni maelekezo gani aliyoyakubali Adamu na kutoka kwa nani, ambayo yalimfanya kupokea roho iliyoungana na roho yake ili kumpa ufahamu?

***"Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwaa chakula…basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe*** *{Adamu}****, naye akala" Mwanzo 3:6.*** Tuko pamoja wapendwa? Roho iliyoungana na roho ya Adamu kumpa ufahamu wa jinsi ya kuishi ni roho ya Shetani mdanganyifu; ***"…roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi" Waefeso 2:2.***

Basi je! ni roho hiyo ya Shetani ndiyo ambayo wewe pia uliipokea? Kwa hakika hakuna atakayejibu ndiyo! Lakini fahamuni kwamba; kuna tofauti kubwa kati ya kusema na kutenda.

Tunaitambua roho iliyo ndani ya mtu kwa matendo yake na wala si kwa maneno tu ya kinywa chake; vile vile ambavyo imani *{kile alichokubali mtu}* huthibitishwa kwa matendo. Kwa hivyo tafadhali, usiharakishe kujibu kwa blaa blaa tu! Uchunguze moyo wako kwa umakini na unyenyekevu mkubwa, ili uone kile ulichokipokea kama ufahamu, ambacho pia ndicho ukitendacho; maana, ***"kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake" Mathayo 12:34.*** Kisha nenda katika matunda ya roho mbili tofauti *{yaani, roho ya Mungu, na roho ya Shetani}*; uone ni matunda ya roho ipi uliyonayo wewe; soma ***Wagalatia 5:19-21*** ambayo ni matunda ya roho ya Shetani; ulinganishe na ***Wagalatia 5:22-23*** ambayo ni matunda ya roho ya Mungu.

Katika mfumo huo wa Kishetani; mwanadamu ameukubali uongo kwamba yuko sawa na Mungu; kwa maana kwamba, yeye ni mkamilifu, mwenye ufahamu wote, na hivyo kwamba hamwitaji Mungu kwa mwongozo wala cho chote kile; maana anaweza kupanga maisha yake mwenyewe na yakawa sawa tu!

## MATOKEO YAKE

***"Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake" {1 Yohana 1:5}.*** Tunafahamu kwamba dhambi, ambayo ni kinyume cha haki ni giza, na kwamba giza na nuru kamwe havikai pamoja. Basi baada ya Adamu kuchagua kutotii *{uasi}*, Mungu naye ***"akamfukuza bustanini" {soma Mwanzo 3:24}.*** Naam; giza likajitenga na nuru, maana haviwezi kuishi pamoja. Na hali hiyo ikaendelea mpaka sasa kwa uzao wa Adamu; maana Kristo alipokuja alilithibitisha hili akisema; ***"…kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru, wala haji kwenye nuru, matendo yake yasije yakakemewa*** *{vile vile kama Adamu alivyojificha baada ya kula matunda aliyokatazwa kula; Mwanzo 3:11}****" Yohana 3:20.*** Haya yalitokea kabla Adamu hajapata ufahamu kumhusu Mungu na maisha yake, wala kumhusu yeye mwenyewe na maisha yale apaswayo kuishi kwayo. Na kwa vile kile alichokipokea akidhani ni ufahamu kilikuwa uongo; basi, *"akili yake ikatiwa giza, akatengwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga ulio ndani yake, na ugumu wa moyo wake"* ***{soma Waefeso 4:18}.***

Katika ujinga wake, mtu akaanza maisha ya uhuru *{ambayo kimsingi hayawezekani mpaka pale Mungu atakapomfanya kuwa kiumbe wa roho. Wengi hawajui kwamba ni Mungu ndiye huwahifadhi ama kuwalinda hata wenye dhambi}*; lakini yakiendeshwa na Shetani akiwa nyuma ya pazia pasipo mtu kujua. Katika maisha hayo, watu hudhania kuwa wako kama Mungu. Na kwa dhana hii; mwanadamu hatafuti umilele, maana anao tayari; hatafuti kutokufa, maana yeye ni kiumbe wa roho ndani ya mwili wa damu na nyama; wala hatafuti ufahamu, maana anajua kama Mungu! Dhana hii imempeleekea kupigana kujaribu kuufanya uongo aliouamini uonekane kama ukweli. Hebu tulithibitishe hili tafadhalini.

Yale ambayo Adamu aliyapokea kutoka kwa Shetani, ndiyo yale aliyowarithisha uzao wake mpaka kizazi hiki cha sasa. Angalia karibu watu wote leo. Ni kitu gani watu wanachokiangaikia na ni kwa namna gani wanaenenda katika mapambano hayo? Kila mmoja

anapigania kuwa tajiri zaidi *{amiliki vitu vyote kama Mungu anavyomiliki}.* Kila mmoja anataka aonekane kuwa mwenye hekima zaidi *{kama Mungu alivyo mwenye hekima zaidi}.* Tunapambana kujionesha kuwa imara na wenye nguvu zaidi *{kama Mungu alivyo mwenye nguvu zaidi na mkuu}.* Tunapigania kuwa viongozi *{kama Mungu alivyo kiongozi wa vyote}.* Yaani cho chote kile katika maisha, utaona kila mmoja anataka kujionesha kuwa juu ya wengine. Na hii yote ni kutaka kuthibitisha kwamba Shetani hakuwadanganya kwamba wako kama Mungu alivyo!

Matokeo yake sasa; kwa vile lengo la Shetani ni kuwaua wanadamu wote kama ikiwezekana; mataifa yote ya wanadamu yako kwenye machafuko kwa kila mmoja kumwinukia jirani yake akitaka kuwa Mungu wake! Ni nani amewafundisha hayo? Ni Shetani! Sasa basi; kwa mfumo huu, mwanadamu ana imani kwa nani? Bila shaka ni kwa Shetani! Ndiyo maana katika hayo yote, Mungu anawaambia wanadamu kwamba ***"wamerithi uongo, ubatili na vitu visivyofaa, na hivyo ni wajinga!" {soma Yeremia 16:19; Warumi 1:22}.*** Tena kwamba; ***"wote wamepotoka*** *{si baadhi}****, hakuna afahamuye, hakuna mtenda mema hata mmoja" {Warumi 3:11-12}.***

Basi haya yanathibitisha kwamba, hatuko vile tujidhaniavyo na kujichukulia kuwa; na kumaanisha pia kwamba hatufanyi yale tupaswayo kufanya katika maisha haya ya mwili wa nyama na damu. Na kama tulivyokwishaona awali, kwamba mwanadamu hawezi kuishi maisha ya uhuru baada ya kumwacha tegemeo lake *{yaani, Mungu}*; alianza kutegemea vile ambavyo akili yake ya kimwili inavifahamu. Vitu gani? Wanadamu wenzie waliodanganyika kama yeye; kuwashawishi wengine kuwa ni wenye kutegemewa; eti kwa vile wana utajiri, ama kwa vile ni viongozi, au kwa vile ni wenye nguvu! Tukiyatazama haya tukiri tu kwamba, mfumo huu hauna Mungu ndani yake mahali po pote.

## VITENDO VYAUDHIHIRISHA UONGO

Kwa vile Mungu hasemi uongo kamwe; basi baada ya kujihusisha katika mfumo huo, wanadamu na vile wanavyovitegemea pamoja na wao kutegemeana wenyewe, wamekata tamaa; jambo linalouthibitisha mfumo huo kuwa wa uongo, na kuthibitisha pia kile Bwana wetu asemacho kuwa ***"Hakuna mtu awezaye kumkomboa ndugu yake, wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake…ili aishi siku zote asilione kaburi*** *{mauti}****" Zaburi 49:7-9.***

Kwa hivyo; hali hiyo inawathibitishia kwamba wao si miungu bado, na wanakufa; na hivyo pia kwamba hawategemeki, kinyume na ule uongo wauaminio uwaambiavyo! Na pia; utajiri wanaowekeza kwao hauna maana, kwa sababu, ***"Kama kondoo wamewekwa kwenda kuzimu, Na mauti itawachunga…hao wanaozitumainia mali zao, Na kujisifia wingi wa utajiri wao;…hupotea…Na kuwaachia wengine mali zao" Zaburi 49:14,6,10.***

Yale madai kwamba wanafahamu kama Mungu pia yanadhihirika wazi kuwa ya uongo; maana wapangapo mipango yao huku wakitazamia matokeo mazuri, mambo huwa kinyume. Naam; ***"…twatazamia nuru, na kumbe! latokea giza; twatazamia mwanga, lakini twaenenda katika giza kuu. Twapapasa-papasa kutafuta ukuta kama kipofu,..kama watu wasio na macho; twajikwaa wakati wa athuhuri, kana kwamba ni wakati wa ukungu wa alfajiri…Sisi sote twanguruma kama dubu; twaomboleza kama hua; twatazamia hukumu ya haki, lakini hapana, na wokovu, lakini u mbali nasi" Isaya 59:9-11.***

Ni kwanini tunapata matokeo yaliyo kinyume na matarajio yetu? Ni kwa sababu; ***"wamelikataa neno la BWANA*** *{mwongozo pekee wa maisha}**, wana akili gani ndani yao? Yeremia 8:9.*** *{Agiza pia ujumbe wetu usemao,* ***"KATIKA KUTAFUTA AMANI",*** *una maelezo ya kina zaidi; utatumiwa bure}.* Maana, kwa kuukubali uongo kwamba tunao ufahamu tayari na hatuna haja ya kupata ufahamu kutoka kwa Mungu; ***"tumepumbazika; hakuna mwenye ufahamu hata mmoja" {soma Warumi 1:22; 3:11}.*** Hali hii imewaacha wanadamu katika giza nene! Maana mtu anamtegemea mwanadamu mwenzie, alafu ghafla! mtu huyo aliyemtegemea anakufa, ama kutomsaidia. Mwingine anategemea utajiri, lakini ***"mali hazifaidii kitu siku ya ghadhabu" Mithali 11:4.***

Tena; mwingine hutegemea nguvu zake za mwili, ama nguvu za rafiki yake; lakini ghafla kwa ugonjwa ama ajali, mtu huyo huonekana asiyejiweza akiendeshwa na baiskeli au kitanda cha magurudumu! Tajiri, mwenye nguvu, ama kiongozi; anakabiliwa na magonjwa, ajali, uvamizi, na hata majanga ya asili vile vile kama anavyokabiliwa masikini, dhaifu, ama aongozwaye! Naam; anakufa na kuuacha utajiri; ama utajiri unakwisha *{anafilisika}* na kubakia bila kitu.

Lakini pamoja na uthibitisho wote huu; bado mwanadamu ameendelea kupigania na kuendelea katika mfumo huu huu wa uongo kwa sababu ni kipofu kweli kweli. Tunaendelea kushindana na wengine kutafuta kuonekana kuwa wakuu juu yao; tunaendelea kutegemeana, kutumaini mali na hivyo kumnyima Mungu nafasi ya kutuumba na kutufanya viumbe wakuu ambao Shetani ametudanganya kuwa tumekwishafanyika tayari!

Basi ni kwa upofu huu wa kuyakataa maisha kama yaelezwavyo na sheria za Mungu, kwamba wanadamu wamefikia hali hii mbaya ya karibia kutoweka kama tushuhudiavyo kote ulimwenguni. Sasa basi, kwa vile mwanadamu hawezi kutatua matatizo yake mwenyewe, na sasa kilichosalia kwake ni kutazama tu bila msaada wo wote awezao kufanya; huku pia hali ikizidi kuwa mbaya; je! ni kumaanisha kwamba hakuna tumaini lo lote la kutoka kwenye haya?

## MJUMBE WA MUNGU

Sasa basi; kwa vile matokeo ya kile tukitumiacho kama ufahamu katika maisha tuishiyo yanaonekana na kuthibitishwa wazi kwamba huo si ufahamu; huku Mungu pia akituambia kwa

hakika kuwa huo sio ufahamu, bali ni uongo wenye malengo ya kutuua; je! tuko tayari kujaribu kitu kingine kilicho tofauti endapo tutafunuliwa? Naam; kwa vile kile tulichojenga imani yetu juu yake kimeshindwa; je! tuko tayari kupokea ufahamu mpya wa namna ya kuishi?

Ikiwa tuko tayari; basi jambo la kwanza ni kuutupilia mbali ule uongo, na tukubali kwamba hatuna ufahamu ***{soma 1 Wakorintho 3:18 tafadhali}.*** Hii itafanyiza nafasi akilini mwetu ya kuweka maelekezo mapya ***{soma Mathayo 18:2-3}.*** Je! ni hili ndilo tulilolifanya tukawa wamwabuduo Mungu wa leo? Usiwe mwepesi wa kujibu; maana najua wengi wetu tutajibu ndiyo. Lakini nakusihini kuwa kimya mpaka kwanza umeuchunguza moyo wako kwa nuru ambayo Mungu anaifunua hapa, kisha jibu lako litokane na nuru hiyo ndipo litakuwa jibu la uhakika.

Kile Mungu alichokusudia kukifanya, ni sharti akitimize; maana anasema, ***"…mimi nitatenda kazi, naye ni nani awezaye kuizuia?" Isaya 43:13.*** Kwa msimamo huo, huku kipaumbele chake kikiwa ni kuurejesha tena Ufalme wake hapa duniani, tena kupitia kwa mwanadamu *{agiza ujumbe wetu usemao, **"MCHAKATO WA UUMBWAJI WA MTU",** kwa maelezo zaidi, na utatumiwa bure}*; Mungu alimtuma mjumbe wake, Yesu Kristo; kumrudisha mwanadamu nyuma mpaka pale Adamu alipobakia. Maana anatuambia; ***"…Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu…" Yeremia 6:16.***

Kumbukeni; Mungu ananena na mimi pamoja na wewe hivi sasa. Hebu tufanye hivyo atuambiavyo. Na kwa kufanya hivyo; ni kitu gani tumekiona katika hiyo njia ya zamani? Kwa hakika; ni maagizo yaliyo tofauti kabisa *{kuhusu Mungu na maisha yake; kumhusu mwanadamu na maisha yake; na kuhusu umiliki wa vitu/mali na mathumuni yake katika maisha}*, ambayo endapo mtu atayasikiza na kuyakubali, yatajenga ndani yake ufahamu mpya na kumpa aina mpya ya imani inayokubalika.

Sasa basi; ni nini asemacho mjumbe kutuhusu sisi na maisha yale tupaswayo kuishi kwayo kama yalivyokusudiwa na Muumba wetu, ambayo kama yakifuatwa yataleta yale maisha yatamaniwayo na kuonekana kama ndoto? Lakini kabla ya kwenda katika hilo; hebu tukumbukeni tafadhali kwamba; kwa mujibu wa maisha ya sasa; imani ile tuliyoikataa, ni kwamba mwanadamu ni roho kama Mungu, bali aishiye ndani ya mwili wa nyama na damu *{yaani ni mwili na ni roho}.* Kwamba, amekamilika kwa kuwa na uwezo, umiliki, uongozi, bora zaidi na kadha wa kadha ambazo ni sifa za Mungu ndivyo mwanadamu alivyo! Kwa mujibu wa imani hiyo; mtu ni sharti apigiwe magoti na watu wenzake, awashauri wengine, aheshimiwe na kutiiwa, ajulikane na kufuatwa na wengine. Kama tulivyokwishaona, imani ya aina hii imeshindwa kabisa; na sasa tumemrejelea Muumba wetu baada ya kugundua kile Shetani alichotutenda *{hapa nazungumza sasa na wale waliyoyafumbua macho yao}.*

Wakati alipokuja mjumbe wa Mungu, hiki ndicho alichokifunua ama kudhihirisha, na anaendelea kufanya hivyo hivi sasa kwa wale wayatakao maisha bora yenye utimilifu wote.

Sikiza tafadhali, na uone kama unajifahamu kwa namna hii. Ingawa Mungu anamtaka mtu aliye kama yeye katika namna zote, lakini hakumuumba mara moja kwa kiwango hicho. Mjumbe wake anatuthibitishia kwamba hivi sasa sisi sote tu *"mavumbi, wenye maisha mafupi; tunaohitaji kupata ufahamu kwa kujifunza kwake; ambao ili kuendelea kuishi, ni sharti tumtegemee Mungu; tulio katika mchakato wa kufanywa kuwa kama Mungu; tusioweza kufanya lo lote pasipo msaada wa Mungu; sote tuko sawa kwa kiwango kimoja; na ambao tuko katika mwili huu ili kutafuta heshima, utukufu na kutokuharibika, yaani uzima wa milele {naam; hatuko kama Mungu isipokuwa kwa mfano wake tu; agiza ujumbe wetu usemao "KUSUDI LA MWILI" kwa maelezo zaidi}; tafadhali soma* ***Mwanzo 3:19; Ayubu14:1-2; Waefeso 4:23; 1 Wakorintho 3:18; Waefeso 4:24; Yohana 15:5; Warumi 2:7****}.*

Basi ye yote anayedai kuwa na imani kwa Mungu ni lazima ajifahamu kwa hayo yaliyohainishwa hapo juu, na wala si kwa yale tuliyoyafahamu kutoka kwa Shetani.

## IMANI YA KWELI

Kumbukeni; sababu ya kuwa na imani ni ili kutuongoza katika hatima yetu ya kufanywa miungu; naam, kufanywa viumbe wa roho ili tutawale katika Ufalme wa Mungu tukiwa washirika wa Familia yake, tukishiriki maisha ya utukufu wake. Kumbukeni pia kwamba; baada ya Mungu kuanza mchakato huo; mwanadamu alidanganyika katika hatua ya kwanza ambayo pia ilisitisha mpango wa Mungu, na kumwacha akitafuta ***"vitu visivyomfaa" {Yeremia 16:19}.***

Hapa basi; Mjumbe wa Mungu amekuja na *"kuyafungua macho yetu katika mafunzo sahihi, ili tukiyakubali turejee katika ramani halisi ya Mungu {soma* ***Isaya 42:6-7****}.* Basi je! wewe u miongoni mwa walioukubali na kuuamini ujumbe wake? Tunathibitishaje? Naam; ni kitu gani tunachohitaji kuona nafsi zetu zikifanya ili tuwe na hakika kwamba tumepiga mbio katika mafunzo ya Mungu kuhusu kusudi la maisha yetu? Kile Mungu asemacho hapa ni thabiti kwa wale ambao mioyoni mwao inakaa roho takatifu, ambayo pasipo hiyo, hakuna awezaye kuyaelewa haya! Maana akili ya mwili inaelewa mambo ya mwili pekee ***{1 Wakorintho 2:14}***; kwa hivyo, tunapojaribu kuitumia kufahamu njia ya maisha ya Mungu, tunajichanganya tu, maana hayafahamiki! Akili ya mwili pia inayakataa maisha ya roho ***{Warumi 8:7}.*** Ndiyo sababu kila tujaribupo kutii sheria za Mungu kwa akili ya mwili, zinaonekana kuwa mzigo mzito; na hivyo tunachoambulia ni kujionesha *{kuwa watiifu}* kwa nje tu ilhali mioyo na mienendo yetu iko kinyume kabisa.

Kwa hivyo basi; wale waliomwamini mjumbe wa Mungu kweli kweli, wanalitambua hili kwamba, ***"tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu*** *{mchakato wa uumbwaji ukiendelea, haujakamilika bado}****, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo" Waefeso 2:10.*** Kwa sababu hii; tunakubali pia unyonge wetu; naam, jinsi tusivyoweza kujijenga hata kwa inchi moja, tukikubaliana na mjumbe kwamba, ***"pasipo yeye hatuwezi kufanya cho chote" {soma Yohana 15:5; Zaburi 127:1}.***

Tumekubali pia kwamba tu wajinga, tusiojua cho chote kuhusu sisi ni nini, kwanini tupo, na ni nini hatima yetu. Na hili linatufanya *"kumtumaini Mungu kwa mioyo yetu yote; na kutokufanya mambo kwa mawazo yetu wenyewe {maana hatuna ufahamu}; bali kwa uelekevu kusikiza kile Mungu asemacho {kwa kusoma Biblia} kuhusu cho chote tutakacho kufanya kila wakati {**Mithali 3:5-6**}.* Basi je! hivi ndivyo tufanyavyo na hivyo kujitambua kama wamwabuduo Mungu halisi?

## THIBITISHA

Ikiwa kweli tumefikia kiwango hiki katika kumtegemea Mungu; ni sharti tutahainisha mabadiliko kadha wa kadha katika maisha yetu. Jitazame mwenyewe kama unayaona mabadiliko hayo; na kama hayapo, tambua hakika kwamba ungali katika udanganyifu wa awali, na kudhania tu kile kisicho ndani yako. Na kisichokuwepo ni hali ya utupu.

Kwa hivyo; ye yote aliyeusikia ujumbe wa Mungu ukihubiriwa na Kristo, ni lazima aanze kwa kujifahamu nafsi yake kuwa si kitu ***{Wagalatia 6:3,1}***; maana ndivyo ujumbe usemavyo; na kwa sababu hiyo, mtu ni lazima pia ajikane nafsi kikamilifu *{yaani kuyakana yote aliyoyatumia hapo kabla kama njia ya maisha; **Mathayo 16:24**}.* Basi fahamuni ya kwamba huu ni mwanzo na si mwendelezo. Kwanini? Kwa sababu kile tulichopokea na kudhania kuwa ni mwanzo kilikuwa uongo! Adamu alibakia kwenye kiwango alichoishia Mungu katika kumuumba; yaani wa mwili wa nyama na damu, mwenye maisha mafupi yapoteayo, tena mjinga!

Ni nini basi? Ni kitu gani anachokitangaza Kristo, tulichokisikia, na hivyo kuwa na imani nacho *{kumbuka kusoma ujumbe wetu usemao **"MCHAKATO WA UUMBWAJI WA MTU"** kwa maelezo ya msaada zaidi}*? Naam; jengo halijitambui, wala kujua jinsi mjenzi atakavyo liwe. Halipingi, halipendekezi wala kuongeza cho chote, isipokuwa tu kwenda sawasawa na afanyacho mjenzi. Maana; ***"kama udongo ulivyo katika mkono wa mfinyanzi, ndivyo tulivyo mkononi mwa Mungu" {Yeremia 18:6}.*** Hapa ndipo wanaposimama waabuduo halisi wa Mungu, baada ya kuupokea ujumbe autangazao Kristo. Hatujifahamu kwa namna yo yote ile, isipokuwa kwa kile tusomacho katika maandiko; maana, *"maandiko hayo {sheria} ndiyo ufahamu, hekima na akili yetu" {soma Torati 4:6}.* Na maandiko hayo yanasema; ***"…wote wenye mwili ni majani…ni kama ua la kondeni…" Isaya 40:6-7.***

Basi kwa kuwa na ufahamu huu; waabuduo halisi hawakubaliani na kile wanachohisi ama kudhania kuhusiana na nafsi zao wenyewe, wala hawakubaliani na kile watu wasemacho ama kuwadhania. Tunalo wingu la mashahidi, kuanzia kwa Kristo mwenyewe ambaye *"hakujali cheo cha mtu, wala kutazama sura ya mtu {akianzia kwake mwenyewe; **Yohana 7:16-17**}"* ***Mathayo 22:16.*** Tena; *"hakujitumainisha kwa watu; maana anawajua watu wote pamoja na yale yaliyomo ndani yao" {**Yohana 2:24**}.*

Wote waliouamini ujumbe wake walienenda vile vile kama yeye. Kwa mfano Paulo na Petro walirudia yale yale aliyoyasema Yesu, wakisema; ***"…au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo" Wagalatia 1:10.*** Tena; ***"…Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu" Matendo 5:29.*** Naam; tena, ***"…kwangu mimi, si kitu kabisa nihukumiwe na ninyi, wala kwa hukumu ya kibinadamu, wala sijihukumu hata nafsi yangu" 1 Wakorintho 4:3.*** Kwanini? Mungu ameeleza wazi katika ujumbe huu kwamba mbali na mfumo wake wa maisha kwa wanadamu; wanadamu hawafahamu cho chote; na mbali na ufahamu wa Mungu; *"moyo wa mwanadamu ni mdanganyifu, usiofahamu wala kumtii Mungu"* ***{soma Yeremia 17:9; 1 Wakorintho 2:14; Warumi8:7}.***

Kwa hivyo; waabuduo halisi wa Mungu hawajihesabu, wala hawawahesabu watu wawazungukao katika maisha yao mapya. Wanafahamu kwamba wao pamoja na hawa wawazungukao *{jamii yote}* hawajui cho chote; na kwamba Mungu ndiye ajuaye, na hivyo ndiye pekee asemaye ukweli. Kwa sababu hiyo; hawafurahii kusifiwa na watu, wala pia hawakwazwi na dharau zao ***{Luka 6:26,22}***; maana wanajua jinsi moyo na wanadamu wanavyoongea kulingana na ujinga walionao, na vile kusivyokuwa na ukweli ndani yao. Je! hii ndiyo imani uliyonayo? Je! huu ndio ufahamu ulionao kujihusu? Hawa waabuduo halisi wa Mungu wanafahamu pia kuwa huu mwili na maisha yake ni nini *{yana kusudi gani}*, na hivyo hawatafuti kuulinda, maana wanafahamu wakati fulani utakufa. Naam; wako makini katika *"kumtafuta Bwana, wakiacha na kusahau njia zao mbaya za awali walizojidhania"* ***{Isaya 55:6-7}.*** Naam; kwa hakika, ***"wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika…" Warumi 2:7.***

Wingu la mashahidi wetu wanalithibitisha hili; maana wote walikufa pasipo woga wala majuto. Hawakuthubutu kujaribu kuulinda mwili, maana wanaufahamu kuwa ni sehemu ya kwanza tu ya hatua ya uumbwaji ambayo kama hawatasalia mikononi mwa Muumbaji, utapotea. Mtazame Kristo msalabani; Shadraka, Meshaki na Abednego ndani ya moto; Danieli katika tundu *{shimo}* la simba; Stefano akipigwa mawe; ni wingu la mashahidi kweli, waliojikana kweli pasipo kujali miili yao, maana walijua makusudi ya maisha ya mwili huu *{agiza ujumbe usemao **"KUSUDI LA MWILI"** kwa maelezo ya msaada zaidi}.*

Basi je! haya ndiyo maelekezo tuliyoyapata kwa Kristo na kuyakubali, na hivyo kuwa na imani nayo? Hawakusumbuliwa na utajiri wala umasikini. Mtazame Ibrahimu. Sidhani kama kuna mtu duniani leo mwenye utajiri wa kulinganishwa na wa Ibrahimu! Lakini pamoja na yote hayo; Ibrahimu akaishi maisha ya shauku *{kiu}* moyoni, ***"akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo,..akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu" Waebrania 11:9-10.*** Naam; hakuiangalia mali moyoni mwake; maana alijua haiwezi kumjenga na kumfanya kiumbe wa roho ***{soma Zaburi 62:10; Mathayo 6:19-20}.***

Mtazame Danieli ambaye hakuwa tajiri; lakini pindi mfalme Belshaza alipomwahidia zawadi ya vitu na ukuu, Danieli hakushawishiwa navyo, na akamwambia mfalme; ***"…Zawadi zako zishike wewe mwenyewe; na thawabu zako mpe mtu mwingine…" Danieli 5:17.*** Ni nani

miongoni mwa wahubiri wa leo awezaye kukataa zawadi namna hii? Na ni kwanini Danieli yeye hakuona thamani ya utajiri huo? Ukimzungumzia Petro, pamoja na wote waliomwabudu Mungu katika kweli; walifahamu *{kwa maelekezo waliyoyapokea na kuyakubali kutoka kwa Mungu}* kwamba uhai huu hausababishwi ama kutokana na utajiri, wala jitihada zo zote za kimwili; bali unatokana na Mungu aliyetuumba ili tufikie hatima yetu ya kufanyika viumbe wa roho. Kwa kuyathibitisha haya, Kristo anasema; ***"…uzima** {ama uhai} **wa mtu haumo katika wingi wa vitu vyake alivyo navyo" Luka 12:15.***

Mtazame Paulo aliyekuwa masikini; lakini moyo wake kamwe haukulilia utajiri, ***"bali kuvikwa** {mwili wa roho}, **ili mwili huu** {wa damu na nyama} **upatikanao na mauti umezwe na uzima" {2 Wakorintho 5:4}.*** Naam; waabuduo halisi wa Mungu hawakukubali kisifiwa na watu. Daima walikuwa makini kuhakikisha kwamba Mungu atuumbaye ndiye anatukuzwa na kuinuliwa katika yote yafanyikayo maishani mwao. Maana kwa kuwa mjenzi pekee; *"kila kilicho chema chatoka kwake"*. Maana ***"tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili dhamana kuu ya uwezo iwe juu ya Mungu, wala si kutoka kwetu…Maana ni nani anayekupambanua na mwingine? Nawe una nini usichokipokea? Lakini iwapo ulipokea, wajisifia nini kana kwamba hukupokea?" 2 Wakorintho 4:7; 1 Wakorintho 4:7.*** Tunamaanisha nini hapa basi? Maisha ya waabuduo halisi wa Mungu hayajengwi juu ya cho chote ambacho maisha ya ulimwengu huu *{ambayo ni udanganyifu wa Shetani}* hutegemea.

## JIBU

Tuliuliza swali awali mwanzoni mwa ujumbe huu; na tukashauri kwamba tusitoe majibu mpaka tutakapokuwa tumesoma kile ambacho ujumbe huu unaelekeza. Sasa tunahitaji majibu tafadhali. Mnalikumbuka swali lenyewe? Hebu niwakumbusheni. Tukijitambua ya kuwa tuko katika hatua ya kwanza ya mchakato wa uumbwaji wetu ambayo ni ya mwili; na ambayo uumbwaji wake ni Mungu pekee aufanyaye; na kwamba anaufanya sawasawa na asemavyo katika neno lake; kwamba tumeumbwa katika neno hilo *{ni maisha yetu}*; na kwamba hatua inayoendelea hivi sasa ni ya kupata ufahamu ambao kwa kuufanyia kazi tunajenga tabia *{mwenendo}* ambayo ni kitu kisichowezeshwa kwa utajiri, wala nguvu za mwili, wala kuungwa mkono na watu, wala nyadhifa; jambo liwezeshwalo kwa kufanya tu yale ayasemayo Mungu katika neno lake; je! ni kweli kwamba sasa tumegeuka na kujitiisha kikamilifu katika ufahamu huu? Je! hii ndiyo Imani tuishiyo kwayo na kuthibitisha kuwa tu uzao wa manabii na mitume waliojifunza kwa Kristo ***{Waefeso 2:20}***?

Tafadhali soma ***Waebrania 11*** sura yote, uone wingu la mashahidi wetu waliofaulu kikamilifu kuifuata imani mpaka mwisho. Walijitoa nafsi zao kutii neno la Mungu katika hali yo yote ile kwamba ni hasi au chanya *{katika hali mbaya au nzuri}* kwao. Hawakuugeukia mwili, wala jamii iliyowazunguka katika kufurahi ama kuogopa kulingana na mwili. Walikuwa na Mungu na neno lake pekee kama ***"hofu na utisho wao" {soma Isaya 8:13}.*** Kwanini? Kwa

kuwa ndiye pekee awezaye kutuumba mpaka ukamilifu, katika utukufu ule usioharibika. Naam; utukufu ule ambao thamani yake hailinganishwi na cho chote kile tulichokipata katika uongo wa Edeni; maana, *"maisha haya ya sasa hayalinganishwi kamwe na utukufu ule ujao tulioahidiwa" {soma **Warumi 8:18**}.*

Basi je! hiki ndicho ulichokisikia kwa Kristo *{Injili ya kweli}* na kukikubali, na hivyo kwamba kama wote waliotutangulia, wewe pia unakitafuta? Je! Imani yako ni kwa Mungu ndani ya Kristo Bwana wetu? Wote wenye imani hiyo wanapoteza vyote walivyovithamini katika mwili; maana wamegundua jinsi visivyoweza kuwafikisha pale wanapopataka; katika maisha ya milele yenye amani, furaha na ukamilifu wote. Hii ndiyo sababu katika kila jambo hufikiria kwanza, *"ni nini asemacho Mungu?"*. Na hata kama jambo litaupeleekea mwili mateso; wanamtii Mungu bila maswali. Ndiyo sababu wanasema; ***"…mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu" Warumi 8:38-39.***

Naam; wanatambua kwamba kama Mungu hatawafanya kuwa vile alivyokusudia tangu mwanzo, kama alivyoelekeza katika neno lake kwa wale wanaomtii; basi ***"kwa hakika watakufa" {Mwanzo 2:17}.*** Kwa vile yote tuyafanyayo ni katika kujiepusha na mateso na kifo; huku ulimwengu mzima ukiwa umedanganywa na wanatafuta kifo huku wakidhani wanajiepusha nacho; sasa basi, kwa vile Mungu ameyafumbua macho yetu na kufahamu njia sahihi ya kuepuka kifo; tumeamini kweli na kwamba hii ndiyo Imani yetu? Tunaweza kujibu swali hili kwa matendo na si kwa maneno matupu! Na ni kwa kufanya tu sawasawa na neno la Mungu katika kila jambo maishani; maana, *"tulapo, au tunywapo, au tutendapo neno lo lote, tufanye yote kwa utukufu wa Mungu" {**1 Wakorintho10:31**}.*

Wapendwa; haya yatawezekana tu kwa kulitumia neno la Mungu katika kila wazo, kila haja, kila hisia, kila tendo na kila neno. Hii ndiyo Imani iliyokabidhiwa mara moja tu kwa watakatifu; yaani, ukubali wa maelekezo ya Mungu kuhusu sisi ni nini, kwanini tupo, na nini hatima yetu *{ambayo ni kile tulichokielezea katika ujumbe huu}*. Watangulizi wetu katika kuthibitisha imani yao kwa Mungu; *"walijitiisha kwa Mungu kwa kila njia {kwa kutenda neno} katika saburi nyingi, dhiki, misiba, shida, mapigo, vifungo, fitina, taabu n.k. {tafadhali soma **2 Wakorintho 6:4-10**}.* Katika hali zote; haikuwa kazi yao kufikiria kile kitakachotokea baada ya kuwa wamefanya kile kisemwacho na neno. Walichozingatia wao ni kumtii Mungu, huku wakimwamini na kumwachia yeye jukumu la kushughulika na matokeo, na wala si wao kulinda nafsi zao. Ni imani gani uliyonayo wewe? Je! ni ile inayoukubali uongo wa Edeni, na hivyo kujenga katika mwili na malengo yake; ama ni ile tuliyoifafanua hapa iliyojengwa juu ya neno la Mungu, ambayo kwa wale waitiiyo watakamilishwa na kufanywa wana *{wa kiume na wa kike}* wa kiroho wa Mungu, wakishiriki familia tukufu pamoja naye milele? Basi sasa unaweza kujibu swali hili kwa usahihi kabisa isipokuwa tu kama hukujichunguza na kujithathmini kwa kioo hiki; yaani, ***"sheria kamilifu ya uhuru" {Yakobo 1:24-25}.***

Wapendwa; hii muisikiayo hapa ni sauti ya Kristo, akisihi kwa upendo mwingi, kwamba wale aliowafumbua macho *{kupitia ujumbe huu}* walio katika Laodikia *{utumwa wa kiroho}*, pamoja na wale waisikiao kwa mara ya kwanza wamrudie. Basi; ***"Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo Mchungaji mwema, tena Mkuu, awaambia awapendao!"*** Naam; anapaza sauti hii kupitia kwa watumwa wake, ***Kanisa la Mungu.*** Basi kwa atakayependa kumsikia na kujifunza kwake zaidi awasiliane nasi kwa anuani zifuatazo:-

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Mwanza –** Simu; +255 753 359 179, +255 688 359 179 & +255 655 659 179.

WhatsApp; +255 655 659 179.

Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg

**Arusha –** Simu; +255 754 028 574 & +255 782 422 216.

**Dar Es Salaam –** Simu; +255 762 055 056 & +255 672 611 204.

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

**Nairobi –** Simu; +254 739 434 639.

Barua pepe; endcog@gmail.com

Wavuti; www.endtimecog.org

**KANISA LA MUNGU – UGANDA**

**Kampala –** Simu; +256 754 167 854.